TANGAZO LA SERIKALI NA. 470 la tarehe 14/7/2023

SHERIA YA MWENENDO WA MASHAURI YA JINAI,
(SURA YA 20)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 204(1))*

AMRI YA UTEUZI WA WATAALAM WA PICHA YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uteuzi wa Wataalam wa Picha ya mwaka, 2023.

Uteuzi wa wataalam wa picha

2. Watu ambao majina yao yametajwa kwenye Jedwali la Amri hii wameteuliwa kuwa Wataalam wa Picha kwa madhumuni ya kutoa ripoti kama ushahidi katika mashauri ya jinai au katika mambo yanayohusiana.

Uhalali wa uteuzi

3.-(1) Uteuzi wa wataalam wa picha katika Amri hii utakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitano kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Amri hii.

(2) Bila ya kujali ujumla wa aya ndogo ya (1), mtu aliyeteuliwa kama mtaalam wa picha chini ya Amri hii anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi kinachopungua miaka mitano pale ambapo ajira ya mtu huyo katika utumishi wa umma itakoma au uteuzi wake utasitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| S/N | NAMES |
|---|---|
| 1. | Daniel Mirandu Kasokola. |
| 2. | Lilian Boniface Matho |
| 3. | Seleman Edward Mahinya |

Dodoma
21 Juni, 2023

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU,
*Mkurugenzi wa Mashtaka*